## MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA

***Karatasi ya maswali: namba 7***

Jaribu kuyajibu maswali yafuatayo kwa maneno yako mwenyewe. Pale palipoandikwa ‘Kazi ya ziada’ unaweza kulijibu swali kama ukipenda, au kuliacha kama unaona huliwezi. Tafadhali jaribu kuyajibu maswali mengine yote.

**MASOMO: 24 – 27**

24 A. Eleza jinsi tunavyoweza kuokolewa.

B. Eleza kwa maneno yako maana ya ‘neema’ au ‘rehema’.

Kazi ya ziada
24. C. Nini maana ya: ‘Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi?’ (Warumi 6:1).

25. A. Ni namna ipi sahihi ya kumwelezea muumini wa kweli ambaye ndio amefariki?
    a) Amekufa.
    b) Amekwenda mbinguni.
    c) Amelala usingizi.

B. a) Toa sababu zinazoonesha kuwa Yesu hakuwa ‘roho’ alipofufuka kutoka kwa wafu.
   b) Kazi ya ziada:
      Unaweza kutoa vifungu vingine ukiacha Luka 24, kuthibitisha jibu lako katika (a)? Kama ‘ndio’ vitaje.
   c) Je? Waumini watakuwa na ‘miili’ watakapofufuka kutoka kwa wafu?
   d) Kazi ya ziada: Unaweza kutoa mstari wa rejea kuthibitisha jibu lako katika (c)?

C. a) Katika Yohana, Sura ya 11, Mariamu alisemaje mara tu alipomwona Yesu?
   b) Lazaro alitokaje kaburini?
   c) Katika Yohana 12:10-11 tunaambiwaje kuwahusu makuhani wakuu?

Kazi ya ziada
D. Mistari gani katika Yohana 5 inayosema kuwa:
   a) Mungu ametoa mamlaka yote ya kuhukumu kwa Mwanawe?
   b) Wakati unakuja ambao wote walio makaburini wataisikia sauti ya Yesu?
   c) Kama tunayasikia maneno ya Yesu na kumuamini, tunaweza kupita mauti na kuwa na uzima?

26. A. Yaweke matukio haya katika mpangilio sahihi:
    UFUFUO / KURUDI YESU/ KUUSIMAMISHA UFALME / HUKUMU

B. a) Hebu andika Mathayo 25:31 – 32.
   b) Mwana wa Adamu katika mstari wa 31 ni nani?

c) Mstari wa 34 unasema zawadi kwa 'wenye haki' ilikuwa ni nini?
d) Ni nini ambacho wenye haki walifanya, ambacho wasio na haki hawakufanya?

C. Ni watu gani ambao hawatahukumiwa?